**HOTUBA YA MGENI RASMI, MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. MAGALULA SAID MAGALULA WAKATI WA SHEREHE ZA UFUNGUZI WA TAWI LA NMB SUMBAWANGA ZILIZOFANYIKA 26 FEBRUARI 2016.**

Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu,

Bw. Badru Idd, Meneja wa Kanda za Juu Kusini,

Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM (M),

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Mheshimiwa Mstahiki Meya,

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi wa Taasisi za Kiserikali,

Viongozi wa Mashirika ya Umma na Binafsi,

Watumishi wa Idara mbali mbali za Serikali,

Ndugu Wafanyabiashara na Wateja wa NMB,

Ndugu Wafanyakazi wa NMB,

Ndugu Waalikwa wote

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia Afya na Amani ya kutuwezesha kushiriki katika sherehe za ufunguzi wa jengo la NMB Sumbawanga Mjini. Aidha napenda kuwakaribisha wote waliotoka nje ya Mkoa na Mji huu wa Sumbawanga. Karibuni sana Mkoani Rukwa katika Manispaa ya Sumbawanga.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza na kumtakia Afya njema na maisha marefu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kustaafu salama katika Utumishi wake uliotukuka wa Uwaziri Mkuu. Kwa kweli amekuwa mfano wa kuigwa kwetu sisi na fahari ya kujivunia kwa viongozi

waliotoka Mikoa ya Rukwa na Katavi. Hongera sana Mheshimiwa Mizengo Pinda - Waziri Mkuu Mstaafu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Benki ya NMB ni Benki ambayo Serikali inaitegemea sana katika kufanya malipo katika Taasisi zake zote. Ni Benki ambayo Serikali ina hisa kubwa na ina mtawanyiko mkubwa hadi ngazi ya Wilaya. Katika miaka miwili ya 2014 na 2015, Benki ya NMB imesaidia masuala mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii. Napenda nitaje baadhi ya misaada tuliyopata kutoka NMB kama ifuatavyo:-

(i) Madawati kwa ajili ya shule za Msingi

(ii) Kusaidia uwezeshaji katika Kongamano la Uwekezaji la Novemba 2014 lililofanyika katika Manispaa ya Sumbawanga

Napenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano tunaoupata kutoka NMB Benki. Asanteni sana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Huu sio wakati wa kutoa hotuba. Hata hivyo naomba nitumie nafasi hii kuendelea kuomba msaada wao wa halil na mali kuisaidia Serikali na jamii katika shughuli zinazoendelea katika Mkoa huu wa Rukwa.

Mkoa kwa sasa unaendelea na changamoto za utengenezaji wa madawati na ujenzi wa Maabara. Katika shule za Msingi zinahitaji madawati 80,573 yaliyopo ni 36,994 na upungufu ni43,579 sawa na asilimia 54.1.

Kwa upande wa Shule za Sekondari Mkoa unahitaji meza 28,196 viti 21,793. Ambapo upugufu ni meza 6,439 (22.8%) na vitu 6,403 sawa na (22.7%).

Ni matumaini yangu kuwa NMB itaendelea kusaidiana na Serikali na jamii katika kumaliza changamoto hizi.

Baada ya kusema hivyo napenda sasa kukukaribisha kwa ajili ya kuendelea na taratibu za sherehe hii.

Magalula Said Magalula

**MKUU WA MKOA**

**RUKWA**

## Viambatanishi.

## MAABARA NA MADAWATI

### 1.0 MADAWATI KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Taarifa hii inaonesha takwimu za elimu katika Mkoa za Januari 2016:

### 1.1 ELIMU YA AWALI:

- Idadi ya shule zenye madarasa ya Elimu ya Awali ni 361
- Wanafunzi walioandikishwa elimu ya awali ni 39,546.

### 1.2 ELIMU YA MSINGI:

- Idadi ya Wanafunzi walioandikishwa Darasa la kwanza mwaka 2016 ni wanafunzi 57,046 na bado uandikishaji unaendelea
- Idadi ya madawati ni 41,029
- **Upungufu wa madawati kwa Shule za Msingi**: mahitaji ni 80,573, yaliyopo 36,994 upungufu 43,579

## SHULE ZA MSINGI

| HALMASHAURI | IDADI YA WANAFUNZI | | | MADAWATI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | MAHITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
| SUMBAWANGA (V) | 34,866 | 34,356 | 69,222 | 23,074 | 10,937 | 12,137 |
| NKASI | 30,932 | 32,884 | 63,816 | 21,272 | 9,940 | 11,332 |
| SUMBAWANGA (M) | 27,039 | 29,418 | 56,457 | 18,819 | 8,732 | 10,087 |
| KALAMBO | 25,838 | 26,384 | 52,222 | 17,408 | 7,385 | 10,023 |
| **JUMLA** | **118,675** | **123,042** | **241,717** | **80,573** | **36,994** | **43,579** |

### 1.3 ELIMU YA SEKONDARI:

- Idadi ya shule za Sekondari za Serikali 69
- Idadi ya shule zisizo za Serikali imeongezeka kutoka 5 (2000) hadi 21 (2016) hilo ni ongezeko la shule 16 (320%).

- Shule za Sekondari za Serikali zenye “A Level” ni 10
- Shule za Sekondari zisizo za Serikali zenye Kidato cha Tano na cha Sita ni Nne.
- Idadi ya wanafunzi ni 25,120
- **Upungufu wa samani kwa Shule za Sekondari:** mahitaji ni meza 28,196 viti 28,196 zilizopo meza 21,757 viti 21,793, upungufu meza 6,439 (22.8%) viti 6,403 (22.7%)

## SHULE ZA SEKONDARI

| HALMASHAURI | MAHITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---:|---:|---:|
| KALAMBO | 4,138 | 2,900 | 1,238 |
| NKASI | 6,692 | 4,965 | 1,727 |
| SUMBAWANGA (M) | 11,478 | 9,282 | 2,196 |
| SUMBAWANGA (V) | 5,888 | 4,610 | 1,278 |
| **JUMLA** | **28,196** | **21,757** | **6,439** |

N.B. Taarifa hii yaweza kubadilika kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza wanaoandikishwa.

## 1.0 MIKAKATI

Mikakati ya pamoja imeandaliwa katika kikao cha pamoja kati ya Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala (M), Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Elimu (W) wa shule za Msingi na Sekondari na Maafisa misitu kilichokaa Ofisini kwa Mkuu wa Mkoa tarehe 19 Januari 2016. Na kuazimia kuwa:-

1. Madawati yote yaliyoharibika katika kila shule yakarabatiwe na takwimu za upungufu wa madawati zihakikiwe upya. Kila Halmashauri ianze mara moja kuhakiki idadi halisi ya upungufu wa madawati na kuwasilisha Ofisi ya Mkoa.

2. Kila Halmashauri ianze mara moja kutengeneza madawati ili kumaliza upungufu uliopo, ikiwezekana zaidi ya asilimia 50 ya upungufu iondolewe kabla ya tarehe 31 Machi 2016.

3. Mkuu wa Wilaya ya Kalambo aratibu zoezi la uvunaji wa mbao katika Msitu wa Kalambo eneo la km 6 inapopita barabara ya lami na Mradi wa REA.

4. Zoezi la Utengenezaji wa Madawati liratibiwe na kila Halmashauri kwa kuangalia rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Ikibidi kutafuta mbao katika miti iliyopandwa kwenye maeneo yao kisha kupanda miti mingine mipya.

5. Madawati yatakayotengenezwa yawe yenye mchanganyiko wa chuma na Mbao.

6. Katika zoezi hili wazazi wasichangishwe lakini ikibidi kufanyika michango yoyote katika jamii, lazima jamii ikubaliane na kibali kiombwe kwa Waziri wa Nchi OR TAMISEMI, kupitia kwa Wakuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa.

7. Takwimu kamili ya mahitaji ya madawati itolewe tarehe 31 Machi 2016 mwisho wa zoezi la uandikishaji, lakini zoezi la matengenezo ya madawati liendelee.

8. Ifikapo mwisho wa Mwezi Machi, 2016 kila Halmashuri iwe imetengeneza Madawati nusu ya upungufu uliopo.

9. Taarifa ya awali ya hatua iliyofikiwa ya utengenezaji wa madawati iwasilishwe Mkoani tarehe 31 Machi 2016.

10. Ifikapo mwisho wa Mwezi Juni, 2016 kila Halmashuri iwe imetengeneza Madawati yote na pasiwe na upungufu.

## 2.0 UJENZI WA MAABARA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI:

Kutokana na agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kuhusu ujenzi wa maabara katika Shule za Sekondari za Serikali Mkoa umetekeleza agizo hilo kwa kushirikiana na Halmashauri, Wadau wa Elimu na Jamii.

Mahitaji ya maabara kwa shule za Sekondari za Serikali Kimkoa ni **207**. Maabara zilizokuwepo kabla ya agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni **22**. Maabara zinazotakiwa kujengwa baada ya agizo ni **185**. Kati ya maabara **185** zilizojengwa hakuna maabara iliyokamilika kwa ajili ya matumizi, maabara **152** zipo katika hatua ya umaliziaji, maabara **19** zipo hatua ya linta na maabara **14** zipo hatua ya Msingi zote kutoka Halmashauri ya Wilaya Kalambo.

*Jedwali Na. 16.16: Ujenzi wa maabara katika shule za sekondari za serikali:*

| NA | MKOA | HALMASHAURI | SHULE | MAABARA ZILIZOKUWEPO KABLA YA AGIZO | MAABARA ZILIZOKAMILIKA BAADA YA AGIZO | IDADI YA MAABARA AMBAZO HAZIJAKAMILIKA | HATUA ZA ZILIPOFIKA | SABABU KUTOKAMILIKA KWA UJENZI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | RUKWA | Kalambo | 15 | 3 | 0 | 42 | Maabara 28 zimefikia hatua ya umaliziaji | Uhaba wa rasilimali fedha |
| | | | | | | | Maabara 14 zipo hatua ya msingi | Uhaba wa rasilimali fedha |
| 2. | | Nkasi | 22 | 4 | 0 | 62 | Maabara 2 zimeezekwa | Uhaba wa rasilimali fedha |
| | | | | | | | Maabara 41 zimepigwa kenchi zipo hatua ya kuezekwa | Uhaba wa rasilimali fedha |
| | | | | | | | Maabara 19 zipo hatua ya linta | Uhaba wa rasilimali fedha |
| 3. | | Sumbawanga (M) | 17 | 10 | 0 | 41 | Maabara 41 zipo hatua ya umaliziaji (Plastering) | Uhaba wa rasilimali |
| 4. | | Sumbawanga (V) | 15 | 5 | 0 | 40 | Maabara 40 zipo katika hatua ya ukamilishaji majengo na miundombinu ya ndani | Uhaba wa rasilimali fedha |
| | **JUMLA** | **4** | **69** | **22** | **0** | **185** | | |